# WILAYA YA MAKUENI

## DARASA LA TANO MUHULA WA TATU

PENPLUS MAKUENI

## KISWAHILI

*MUDA: Saa 1 Dakika 40*

***Jaza mianya iliyoachwa wazi kutoka 1-15 kwa jibu sahihi.***

Mwanamume __1__ jana alishtakiwa kwa kosa __2__ __3__ nyaya __4__ simu zenye __5__ ya shilingi elfu sita mjini Maua. Mwanamume __6__ alifikishwa __7__ ya hakimu mkuu wa Maua Bwana Yusuf kwa __8__ ya kuiba nyaya __9__ kwenye eneo __10__ Kingongo mjini Maua mnamo Juni16.

Nyaya __11__ ni mali ya kampuni __12__ simu ya Telcom Kenya. Baada ya __13__ kutekeleza wizi __14__ mwanamume huyo aliagizwa arudi __15__ mnamo tarehe 8 Julai ili kesi yake isikizwe.

1. A. moja B. kimoja C. mmoja D. wamoja
2. A. la B. ya C. wa D. za
3. A. kuimba B. kuiba C. kwiba D. kwimba
4. A. ya B. za C. la D. wa
5. A. dhamani B. damani C. thamani D. tamani
6. A. hii B. hiyo C. hicho D. huyo
7. A. mbele B. chini C. karibu D. nyuma
8. A. mandai B. madai C. madahi D. maadai
9. A. hizo B. hiyo C. hao D. hicho
10. A. wa B. ya C. la D. pa
11. A. hizi B. hizo C. hiyo hayo
12. A. la B. mwa C. cha D. ya
13. A. kukataa B. kuwekwa C. kukana D. kuona
14. A. hio B. hilo C. hizo D. huo
15. A. msikitini B. kanisani C. kortini D. gerezani


***Jibu maswali ya 16 mpaka 30 kulingana na maagizo.***

16. Mtoto wa mwana huitwa ________
    A. kilembwe B. mjukuu
    C. kitukuu D. kinyingiya
17. Malipo kwa ajili ya usafiri huitwa ________
    A. nauli B. karo
    C. faida D. riba
18. ***Tumia kirejeshi 'amba'***
    Kalamu ________ zimepatikana ni zetu.
    A. ambayo B. ambaye
    C. ambazo D. ambalo
19. Zana ya vita iliyochorwa chini ni ________



A. mkuki B. msumani C. mshale D. upote

20. ***Andika tarakimu ifuatayo kwa maneno:- 60829.***
    A. Elfu tisini, mia nne ishirini na sita
    B. Elfu sitini, mia nane ishirini na tisa
    C. Elfu sitini nane mbili tisa
    D. Sita sufuri mia nane na ishirini na tisa
21. Miti, nyasi, mimea,visima hukauka msimu wa ___
    A. masika B. vuli C. kiangazi D. kipupwe
22. Taja maumbo iliyochorwa ________



A. Mraba
B. Pia
C. Hiramu
D. Wimbi

23. ***Kamilisha sentensi.***
    Mama alini ________ picha nzuri sana.
    A. chora B. chorea
    C. chorewa D. choresha
24. Tunasema pofu kama ________
    A. kipofu B. jongoo
    C. mzee D. ajuza
25. ***Andika sentensi kwa wingi.***
    Ng'ombe huyu ndiye aliyeumia
    A. Ng'ombe hizo ndizo zilizoumia
    B. Ng'ombe hao ndio waliyoumia
    C. Ng'ombe hawa ndio walioumia
    D. Ng'ombe hiyo ndiyo waliyoumia
26. Nomino kipepeo liko katika ngeli ya-
    A. KI-VI B. I-ZI C. A-WA D. LI-YA
27. ***Kamilisha methali ifuatayo:-***
    Ukitaka cha mvunguni ________
    A. sharti uiname B. sharti uende
    C. sharti uulize D. sharti uwepo
28. Shairi lenye mishororo minne huitwaje?
    A. Takhmisa B. Tarbia
    C. Tathlitha D. Tathnia
29. Jina jingine la chupi ni ________
    A. kinyasa B. kaptura
    C. kocho D. gagro
30. Kinyume cha **"kushuka"** ni ________
    A. kuteremka B. kukwea
    C. kudandia D. kupaa

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali ya 31-40.***

Watu wawili wanaokabiliwa na shtaka la kudai kuwa wana uwezo wa kiajabu wa kubadilisha shilingi za Kenya kuwa Dola za Amerika jana walimshangaza hakimu walipodai kwamba ni mahakama yenyewe iliyotoa kibali wati we mbaroni.

Wawili hawa wanaokabiliwa na shtaka la kutumia udanganyifu kujipatia pesa walimwambia hakimu mkuu "aondoe kibali cha kuwakamata kwa sababu walifika mahakamani kama walivyoagizwa". Baada ya kukagua faili lao hakimu mkuu alishangaa akisema kwamba hakutoa kibali kwa polisi wawatie mbaroni washtakiwa.

"Nani aliwaambia kwamba nilitoa kibali mkamatwe?" aliwauliza washukiwa walioonekana wanyenyekevu wakiwa kizimbani. Walisema walipotoshwa kwamba mahakama ilikuwa imeagiza wakamatwe.

Mahakama iliambiwa kwamba polisi walikuwa na ushahidi mpya kuhusu kesi inayowakabili na kiongozi wa mashtaka aliomba mahakama ibadilishe mashtaka.

31. Watu wawili walikabiliwa na shtaka la:-
A. kuuwa B. undanganyifu
C. wizi D. kupora
32. Watu hawa walikuwa na uwezo wa ______
A. kubadilisha dola za Kenya kuwa shilingi ya Amerika
B. kuiba pesa za Amerika
C. kubadilisha shilingi za Kenya kuwa Dola za Amerika
D. kuiba pesa za Kenya
33. Kutokana na wahusika nani aliyetoa kibali cha wahusika kutiwa mbaroni?
A. Askari B. Mahakama C. Gereza D. Chifu
34. Neno kizimbani limepigiwa mstari. Inamaanisha:
A. chumba cha nyumba
B. mahali mahakamani mshtakiwa husimama
C. tundu la kuwekea kuku
D. mkahawa
35. 'Kutoa kibali' kulingana na ufahamu ni kumaanisha:-
A. kutoa ruhusa B. kutoa pesa
C. kupewa kitu D. kupewa nafasi
36. Nani alikuwa na ushahidi mpya kuhusu kesi hiyo?
A. Mahakama B. Hakimu C. Polisi D. Raisi
37. Pesa za Amerika huitwa?
A. Shilingi B. Kwacha C. Dola D. Nira
38. Ni watu wangapi walihusika na kesi ndani ya mahakama?
A. Mmoja B. Wawili C. Watatu D. Wanne
39. Kazi ya hakimu ni ______
A. kutoa hukumu B. kupongeza watu
C. kufunga watu D. kupeleka watu kortini
40. Kiongozi wa mashtaka aliomba nini?
A. Kesi iendelee B. Mashtaka ibadilishwe
C. Wahusika wafungwe D. Kesi itupiliwe mbali

***Soma taarifa ifuatayo na ujibu swali la 41-50.***

Barua ya kindugu huandikiwa ndugu na marafiki ili kuwajulia hali na kuwapa ujumbe mbalimbali. Huweza kuwa ndefu au fupi. Urefu wake hutegemea mambo aliyo nayo yule anayeandika. Tofauti na barua rasmi anwani inayoandikwa ni ya mwandishi wa barua pekee upande wa kulia juu pamoja na tarehe.

Mwanzo wa barua hii hutegemea uhusiano wa wale wanaoandikiana. Kwa mfano; kwa mpendwa shangazi/amu, kwa rafiki Suleimani, Babu mpenzi, na kadhalika. Baada ya kukamilisha ujumbe, kiishio huweza kuwa; Ni mimi mwanao mpenzi ni mimi wako sahibu na kadhalika. Si lazima mwandishi aandike majina yake yote kwa vile watu mara nyingi huwa wanafahamiana vyema.

41. Mwandishi ameelezea aina gapi za barua?
A. Tatu B. Mbili C. Moja D. Nne
42. Barua ya kindugu anwani huandikwa wapi?
A. Upande wakushoto B. Upande wa chini
C. Upande wa kulia D. Upande wowote
43. Uandishi wa barua ya kirafiki hutegemea:-
A. Mwandishi B. Ujumbe
C. Wakati D. Karatasi
44. Mwanzo wa barua ya kindugu hutegemea nini?
A. Uhusiano B. Urefu C. Majira D. Uadui
45. Neno **"sahibu"** limepigiwa mstari linamaanisha?
A. Adui B. Rafiki
C. Mwanaume mzee D. Ajuza
46. Kwa nini watu huwa wanaandikiana barua?
A. Hawana fedha za kusafiri
B. Hawawezi kupiga simu
C. Kujuliana hali
D. Kwa kuchukiana
47. Tofauti ya barua rasmi na barua ya kirafiki ni kuwa:-
A. Barua ya kirafiki ni refu kuliko barua rasmi
B. Barua rasmi haina anwani ya mwandishi
C. Barua ya kirafiki haina tarehe
D. Barua ya kirafiki huonyesha anwani ya mwandishi pekee
48. Ni nini sababu ya kutoandika majina yote kwa barua ya kirafiki?
A. Watu wanafahamiana vyema
B. Ukosefu wa kalamu
C. Mtu husahau
D. Watu hawafahamiani kamwe
49. Kinyume cha **"babu mpenzi"** ni:-
A. Babu adui B. Nyanya mpendwa
C. Nyanya adui D. Baba yangu
50. Mojawapo ya njia za mawasialiano mwandishi ameelezea ni ______
A. barua pepe B. kipepesi
C. tarakilishi D. barua